**HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI AKIAHIRISHA MKUTANO WA KUMI WA BUNGE LA 12 LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, TAREHE 10 FEBRUARI, 2023 JIJINI DODOMA**

## UTANGULIZI

### Shukrani

***1. Mheshimiwa Spika***, leo hii, tunapoelekea kuhitimisha shughuli zote zilizopangwa kwenye mkutano wa 10 wa Bunge la 12, tunayo kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya na uzima. Vilevile, tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu atuondolee changamoto za kiafya, ajali na majanga mengineyo na atujalie mafanikio zaidi katika mwaka huu wa 2023.

***2. Mheshimiwa Spika***, Bunge hili tukufu limeendelea kunufaika na weledi, busara, uzoefu na uwezo mkubwa unaouonesha katika kutekeleza majukumu ya Spika wa Bunge. Kipekee, ninakushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuongoza vema Mkutano huu wa Kumi, na hivyo, kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya Bunge hili tukufu katika kuisimamia Serikali.

***3.*** ***Mheshimiwa Spika***, pia, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge ambao wamekuwa na msaada mkubwa kwako **Mheshimiwa Spika** katika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge hili tukufu.

***4.*** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango, maoni na ushauri walioutoa kupitia Mkutano huu wa 10 wa Bunge la 12 ukilenga kuimarisha utendaji wa Serikali. Nikiwa msimamizi wa shughuli za Serikali Bungeni, ninawahakikishia kwamba Serikali imepokea michango hiyo, na itaitumia vema katika kuimarisha utendaji wake.

**Salamu za Pole**

***5.*** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii pia, kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao katika kipindi cha kuanzia Novemba, 2022 hadi sasa kwenye matukio mbalimbali pamoja na ajali za barabarani ikiwemo iliyogharimu maisha ya watu 20 iliyotokea eneo la Korogwe, mkoani Tanga tarehe 04 Februari, 2023 na ile iliyotokea jana tarehe 09 Februari, 2023 katika kijiji cha Silwa, Pandambili, mkoani Dodoma na kupoteza watu 12. Tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za wapendwa wetu mahala pema na awajalie uponyaji wa haraka majeruhi wa majanga hayo. Amin!

**Salamu za Pongezi**

***6.*** ***Mheshimiwa Spika***, hivi karibuni, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya teuzi na mabadiliko ya baadhi ya watendaji wakuu wa taasisi na viongozi hususan kwenye Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mabadiliko hayo yamelenga kuimarisha utendaji na utoaji huduma kwa wananchi.

***7.*** ***Mheshimiwa Spika***, kwanza, ninawapongeza viongozi na watendaji wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kushika nyadhifa mbalimbali. Aidha, katika kuhakikisha wananchi wanahudumiwa ipasavyo, ninasisitiza viongozi na watendaji wote kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais na mipango ya kitaifa katika utekelezaji wa majukumu yao ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026) na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020.

## SHUGHULI ZA BUNGE

### Maswali na Majibu

***8.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mkutano huu, jumla ya maswali **150** ya msingi na mengine **496** ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Halikadhalika,

jumla ya maswali **13** ya papo kwa papo yalielekezwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na yote kujibiwa.

**Taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge**

***9. Mheshimiwa Spika***, kupitia Mkutano huu, Bunge lako tukufu lilipokea na kujadili taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge ambazo zilisheheni maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa Serikali. Nitumie fursa hii kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba Serikali imepokea hoja hizo, itazifanyia kazi na mara utekelezaji wake utakapokamilika, itatoa mrejesho. Aidha, ninaziagiza Wizara zote kufanyia kazi maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Kudumu za Bunge katika kuboresha mipango na bajeti za sekta husika hususan katika kipindi hiki tunachoandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/2024.

**Miswada ya Sheria**

***10. Mheshimiwa Spika***, katika Mkutano huu, pia, Bunge limepokea Mıswada miwili ya sheria ambayo ilisomwa kwa mara ya kwanza. Miswada hiyo ni **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023** na **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2023.**

***11. Mheshimiwa Spika***, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023, utasaidia kuboresha baadhi ya masharti na kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa masharti mbalimbali katika Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi; Sheria ya Huduma za Habari; Sheria ya Bohari ya Dawa; Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa; Sheria ya Reli; Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania; Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani.

***12. Mheshimiwa Spika,*** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2023 utasaidia kuboresha Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na hivyo kuongeza kasi ya ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutaipunguzia Serikali mzigo wa kibajeti sambamba na kukuza sekta binafsi.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA 2022/2023 KATIKA NUSU YA KWANZA (JULAI - DESEMBA 2022)

***13. Mheshimiwa Spika***, hali ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 katika nusu ya kwanza yaani Julai hadi Desemba, 2022 imeendelea kuimarika. Katika kipindi hicho, ridhaa ya matumizi iliyotolewa ilikuwa shilingi trilioni 19.46, sawa

na asilimia 91.7 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 12.29 ni fedha za matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 93.2 ya lengo na shilingi trilioni 7.17 ni fedha za maendeleo, sawa na asilimia 95.1 ya lengo.

***14. Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa mapato ya ndani, makusanyo yamekuwa ya kuridhisha. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2022 mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya halmashauri yalifikia shilingi trilioni 13.40 sawa na asilimia 96.6 ya lengo. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilifanikiwa kukusanya shilingi trilioni 11.68 sawa na asilimia 98.1 ya lengo. Mapato yasiyokuwa ya kodi yalikuwa shilingi trilioni 1.26, sawa na asilimia 86.3 ya lengo na mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 458.6, sawa na asilimia 89.7 ya lengo la kipindi hicho.

***15. Mheshimiwa Spika***, pamoja na mambo mengine, utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/2023 kwa kipindi cha nusu mwaka umewezesha mafanikio yafuatayo:-

**Moja:** Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za Serikali;

**Mbili:** Ukuaji chanya wa uchumi wa asilimia 5.2;

**Tatu:** Utekelezaji wa miradi ya kielelezo ikiwemo ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa, Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere, ujenzi wa daraja la Kigongo - Busisi na uendelezaji wa Mji wa Serikali Mtumba;

**Nne**: Ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ikiwemo ya nishati, barabara, viwanja vya ndege, huduma za jamii, bandari, na kilimo cha umwagiliaji;

**Tano:** Utoaji wa ruzuku kwenye mbolea na bidhaa za mafuta nchini kwa lengo la kudhibiti mfumuko wa bei na kuleta nafuu kwa watumiaji;

**Sita:** Kuongezeka kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya kodi ambapo ukuaji ulifikia asilimia 12.2;

**Saba:** Kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya kukusanyia mapato ambayo imepunguza uvujaji wa mapato katika ngazi zote;

**Nane:** Kutatua hoja nne (4) za Muungano; na

**Tisa:** Kukamilika kwa ufanisi kwa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

***16. Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/2023, changamoto kadhaa zilijitokeza na kuathiri utekelezaji wake. Miongoni mwa changamoto hizo ni ukame uliotokana na mabadiliko ya tabianchi na kuathiri ufugaji wa mifugo, uzalishaji wa mazao na nishati ya umeme, huduma ya maji katika maeneo mbalimbali nchini na uwepo wa sekta kubwa isiyo rasmi ambayo haitozwi kodi ipasavyo. Changamoto nyingine ni mwitikio mdogo wa wamiliki wa ardhi na majengo kulipa ada na tozo kwa wakati; ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuongezeka kwa bei na gharama za usafirishaji wa bidhaa na huduma kutoka nje, hususan bidhaa za petroli, mafuta ya kula na mbolea kulikosababishwa na ongezeko la mahitaji kwenye nchi nyingi duniani.

***17. Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na changamoto hizo ili kuhakikisha malengo ya kiuchumi tuliyojiwekea yanafikiwa. Hatua hizo zinahusisha utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2021; uchimbaji wa visima virefu na mabwawa kwa ajili ya shughuli za kibinadamu na kiuchumi; kuongeza wigo wa kodi kwa kusajili walipa kodi wapya ikiwa ni pamoja na biashara mtandao na usajili wa sekta isiyo rasmi na kuimarisha mifumo ya kieletroniki, kuboresha

taarifa za wamiliki wa ardhi na majengo kulingana na taarifa za sensa ya watu na makazi ili kuongeza wigo wa kodi.

***18. Mheshimiwa Spika***, hatua nyingine ni kuwezesha sekta binafsi kuzalisha kwa tija ili kupunguza utegemezi na uagizaji wa bidhaa kutoka nje na kuendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa biashara duniani ili kuchangamkia fursa zitokanazo na athari za UVIKO-19 na vita ya Ukraine ikiwemo uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula. Vilevile, Serikali inafanya marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ili kuongeza kasi ya ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa PPP na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo wa kibajeti.

***19. Mheshimiwa Spika***, sambamba na hatua zinazoendelea kuchukuliwa katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka, Serikali itaendelea kudhibiti matumizi ili kuendana na mpango na bajeti. Hivyo basi, nitumie fursa hii kuelekeza Wizara na taasisi zote za Serikali kutekeleza masuala yafuatayo wakati wakiendelea na maandalizi ya bajeti ya mwaka 2023/2024:-

**Moja**: Kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/2024 katika maandalizi ya bajeti za mafungu husika;

**Mbili**: Halmashauri zote nchini zenye mapato yasiyolindwa chini ya shilingi bilioni mbili (Kundi C), kuhakikisha zinatenga kiasi kisichopungua asilimia 20 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikijumuisha asilimia 10 ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu;

**Tatu**: Wakuu wote wa Mikoa kuhakikisha wanasimamia kwa karibu miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye maeneo yao ili miradi hiyo iweze kuakisi thamani ya matumizi ya fedha za umma; na

**Nne**: Maafisa Masuuli wote kuzingatia kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2023/2024 ikiwa ni pamoja na kuzingatia kikamilifu Sheria ya Bajeti (SURA 439) na Kanuni zake.

**ELIMU**

***20. Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa elimu, niruhusu nitumie fursa hii adhimu kusisitiza kuhusu masuala machache ambayo ni ujenzi wa miundombinu ya madarasa na uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza na awali kwa mwaka 2023.

**Ukamilishaji wa Miundombinu ya Madarasa na Uandikishaji wa Wanafunzi Kidato cha Kwanza**

***21. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilitoa **shilingi bilioni 160** kwa ajili ya ujenzi wa **vyumba 8,000** vya madarasa katika shule za sekondari ikiwa ni maandalizi ya kupokea wanafunzi wote waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023. Hadi kufikia tarehe 03 Februari 2023 vyumba vya **madarasa 7,874** sawa na **asilimia 98.43** vimekamilika na vyumba vya **madarasa 126** sawa na **asilimia 1.57** vipo katika hatua mbalimbali za umaliziaji.

***22. Mheshimiwa Spika***, ukamilishaji wa ujenzi wa madarasa ya sekondari umewezesha wanafunzi wote **1,076,037** waliofaulu **Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi 2022** kupata fursa ya kupangiwa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwezi Januari 2023 kwenye shule za Serikali kwa awamu moja pekee. ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio haya ni kielelezo tosha cha umakini, uzalendo, maono na kazi iliyotukuka inayotekelezwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kulinda maslahi na kujenga mustakabali mzuri wa taifa letu.

***23. Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kuziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo bado hazijakamilisha ujenzi wa vyumba

vya madarasa kuhakikisha vyumba hivyo vinakamilika kwa wakati. Kadhalika, nitoe wito kwa wazazi wote wenye wanafunzi waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza kuhakikisha kuwa watoto hao wanaripoti kwenye shule walizopangiwa mara moja. Serikali haitosita kumchukulia hatua mzazi au mtu yeyote atakayebainika kumzuia mwanafunzi kupata haki yake ya elimu.

**Uandikishaji wa Wanafunzi wa Darasa la Kwanza na Awali**

***24. Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza na awali tumeendelea kufanya vizuri. Kwa mfano, hadi kufikia tarehe 03 Februari, 2023 **wanafunzi 1,363,320** wa darasa la awali wameandikishwa wakiwemo wenye mahitaji maalum **2,944**. Wanafunzi wote wa darasa la awali walioandikishwa ni sawa na **asilimia 100.18** ya lengo la kuandikisha **wanafunzi 1,360,737**.

***25. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hicho **wanafunzi 1,657,533** wakiwemo wenye mahitaji maalum **3,825** waliandikishwa kwa ajili ya darasa la kwanza sawa na **asilimia 101.29** ya **wanafunzi 1,633,659** waliotarajiwa kuandikishwa. Niendelee kusisitiza kwamba Wakuu wote wa Mikoa hakikisheni wanafunzi wote wenye rika lengwa wanaandikishwa kwa ajili ya darasa la awali na darasa la kwanza kama ambavyo nimeainisha hapo nyuma.

**KILIMO**

**Mwenendo wa Unyeshaji wa Mvua na Hali ya Mazao Shambani Msimu wa Kilimo 2022/2023**

***26. Mheshimiwa Spika***, tupo kwenye msimu wa kilimo na wakulima wameendelea na shughuli za kilimo licha ya baadhi ya maeneo kutopata mvua kwa wakati na wakati mwingine kuwa chini ya wastani. Hali ya mazao katika maeneo yaliyopata mvua za vuli kwa wakati (Septemba na Oktoba) ni nzuri na yamefikia hatua za kuchanua, kubeba na kukomaa na kwenye baadhi ya maeneo wakulima wameanza kuvuna na kuhifadhi mazao kama vile maharage na mahindi. Aidha, katika baadhi ya maeneo mvua za vuli zilianza kwa kuchelewa mwishoni mwa mwezi Novemba na zimeendelea kunyesha na mazao yapo katika hatua ya kukua, kuchanua na kubeba.

***27. Mheshimiwa Spika***, kwa yale maeneo yanayopata mvua za msimu, mvua zimeanza kwa wakati kati ya mwezi Novemba na Desemba, 2022 na mtawanyiko wake umekuwa wa kuridhisha. Hali ilikuwa tofauti kidogo kwa maeneo ya kati mwa nchi ambako mvua hizo zilichelewa kuanza. Hata hivyo, kwa ujumla hali ya mazao shambani ni ya kuridhisha na yapo katika hatua za kuota na kukua kwenye maeneo mengi ya mikoa inayopata mvua hizi.

**Hali ya Upatikanaji wa Chakula Hadi Kufikia Tarehe 31 Januari, 2023**

***28. Mheshimiwa Spika***, hali ya upatikanaji wa chakula nchini imeendelea kuimarika ikichangiwa na uwepo wa ziada ya mazao ya chakula yasiyo ya nafaka yanayojumuisha jamii ya kunde, muhogo, ndizi, viazi vitamu, viazi mviringo, viazi vikuu na magimbi. Vilevile, katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Kagera, Mwanza, Geita na Mara ambayo yamepata mvua za vuli kwa wakati mahindi na maharage yamekomaa na kuendelea kuchangia upatikanaji wa chakula na hivyo, kuimarisha utengamano wa hali ya chakula nchini.

***29. Mheshimiwa Spika***, changamoto kubwa iliyopo sasa ni mabadiliko ya tabianchi, ambapo utabiri wa hali ya hewa umebainisha uwezekano wa mvua chini ya wastani kunyesha kwenye maeneo mengi nchini. Hali hiyo, inaweza kuathiri uzalishaji si tu katika sekta ya kilimo bali pia upatikanaji wa nishati ya umeme, maji, mauzo nje, ukuaji wa uchumi, mapato ya mtu mmoja mmoja, kampuni na Serikali kwa ujumla.

***30. Mheshimiwa Spika***, Serikali katika kukabiliana na hali hiyo imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu ya ugani kwa kilimo cha mazao ya chakula na biashara, kuimarisha kilimo cha umwagiliaji sambamba na

kutoa ruzuku ya pembejeo hususan mbolea ili kuongeza tija na uzalishaji kwenye mazao ambapo hadi Desemba, 2022 tani 175,829.3 zenye thamani ya shilingi bilioni 192.5 zimesambazwa kote nchini.

***31. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Serikali inaendelea na ujenzi wa skimu mpya 25 za umwagiliaji katika maeneo mbalimbali nchini na ukarabati na ukamilishaji wa miundombinu ya umwagiliaji wa skimu 30. Aidha, katika mwaka 2023/2024 na 2024/2025, Serikali imepanga kujenga mabwawa 15 ya kuvunia maji ya mvua ambapo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu na mabonde ya kimkakati unaendelea.

***32. Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine ya kuongeza uzalishaji na tija katika mazao ya chakula na biashara, pamoja na kutengeneza ajira kwa vijana, Serikali kupitia Program ya *Building the Better Tommorow (BBT)* inaendelea na utaratibu wa kuandaa mashamba makubwa (*block farming*) ambayo yatawekwa miundombinu ya umwagiliaji ili kuhakikisha upatikanaji wa maji na hivyo, kuwezesha shughuli za kilimo kufanyika kwa kipindi cha mwaka mzima. Hatua hizi ni muhimu katika kujihakikishia utoshelevu na usalama wa chakula nchini, kuzalisha ajira na pia, chakula cha ziada kwa ajili ya kuuza nje.

**Wito kwa Wakulima**

***33. Mheshimiwa Spika***, kama nilivyotangulia kueleza kwamba nchi yetu imekuwa ikitegemewa katika uzalishaji wa mazao hasa ya chakula kwa ukanda huu. Hata hivyo, nitoe wito kwa wakulima kujenga tabia ya kuhifadhi mazao yao badala ya kuuza yakiwa shambani pamoja na kutumia mifumo rasmi ya kuuzia mazao ili kutokuwa katika hatari ya kukumbwa na upungufu wa chakula siku za usoni. Aidha, niwasihi wakulima kutumia nyenzo rahisi zitakazoongeza thamani ya mazao yao badala ya kuuza yakiwa ghafi kutoka shambani.

## UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

***34. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha hivi karibuni tumeshuhudia kuibuka kwa migogoro mingi ya ardhi ikihusisha mtumiaji mmoja wa ardhi na mtumiaji mwingine katika eneo moja, uvamizi wa kimakundi, madai ya fidia ya ardhi na mwingiliano wa mipaka ya kiutawala na mingineyo. Serikali imekuwa ikifanyia kazi migogoro hiyo hususan ile inayohusu vijiji 975 kupitia Kamati ya Mawaziri Nane wa Kisekta ambayo ilitembelea mikoa yote 26 nchini.

***35. Mheshimiwa Spika***, kwa upande mwingine, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendelea

kubainisha maeneo yatakayomegwa na kurasimishwa kwa wananchi; kutafsiri mipaka ya baadhi ya hifadhi na kuweka alama za kudumu na zinazooneka ardhini; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji vinavyopakana na hifadhi za Taifa; na kufanya tathmini na uthamini kwa wananchi watakaopisha shughuli za uhifadhi kwenye hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Serengeti.

***36. Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine ya kutatua migogoro ya ardhi, tarehe 17 Januari 2023, nikiwa katika eneo la Kapunga, Mbarali niliwafahamisha wananchi kuhusu hatua ya Serikali kufanya maboresho kwenye tangazo lake Na. 28 la Mwaka 2008, kwa kuyatoa nje ya hifadhi baadhi ya maeneo ili kuwezesha wananchi kufanya shughuli za kilimo na ufugaji endelevu. Vijiji zaidi ya 27 na maeneo mengine yanayozunguka Ranchi ya Usangu ni miongoni mwa maeneo yaliyotolewa. Vilevile, Serikali imeitoa nje ya hifadhi, Ranchi ya Usangu ili itumike kwa shughuli za ufugaji wa kisasa badala ya tangazo la awali (GN. Na. 28) ambalo liliingiza ranchi hiyo ndani ya hifadhi.

***37. Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia uamuzi huo ambao umekuwa ni hatua muhimu katika kumaliza mgogoro uliodumu kwa miaka 15. Niendelee kuwataka wananchi kuheshimu uamuzi

wa Serikali na kutimiza wajibu wao ikiwemo utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji kwa maeneo yaliyotengwa na kuridhiwa kwa shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo na ufugaji ikiwemo vijiji vitano vya Luhanga, Madundasi, Kilambo, Iyala na Msanga na Madibila Phase I. Maeneo hayo ni maeneo tegemewa kwa kuzalisha maji kuelekea Mto Ruaha.

***38. Mheshimiwa Spika***, vilevile, ninawakumbusha viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha wanasimamia kikamilifu maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuruhusu wananchi wanaolima kwenye eneo ambalo litabaki katika uhifadhi, kwa msimu huu wa kilimo kuendelea na shughuli zao. Aidha, wote watapaswa kuondoka mara moja baada ya kuvuna mazao yao katika maeneo hayo. Serikali itaendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji. Aidha, wananchi nao wanapaswa kutekeleza wajibu wao wa kuheshimu sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili kuzuia migogoro ya namna hiyo kutojirudia.

***39. Mheshimiwa Spika***, tathmini iliyofanywa na timu ya wataalamu kwenye mikoa 26 imebainisha kuwa ardhi yenye ukubwa wa ekari **1,630,639** imerejeshwa kwa wananchi. Aidha, eneo hilo halijumuishi **ekari 707,962** na **ekari 46,715** kutoka kwenye Mapori Tengefu 12 na Hifadhi za Misitu saba zilizofutwa na ardhi hiyo kurejeshwa kwa wananchi. Hivyo basi, niiagize

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kushirikiana kwa karibu na Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha maeneo hayo yanaandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi ili wananchi waweze kuyatumia kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii na kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo na mifugo na hivyo, kuboresha maisha ya wananchi katika maeneo hayo. Zoezi la Mipango na Matumizi ya Ardhi, lishirikishe wananchi wa maeneo hayo.

**UHIFADHI WA MALIASILI NCHINI**

***40. Mheshimiwa Spika*****,** nchi yetu imejaliwa utajiri mkubwa wa maliasili zikihusisha hifadhi za wanyamapori, hifadhi za misitu na maeneo ya malikale ambazo hatuna budi kuzitunza kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. Hata hivyo, uendelevu wa maliasili hizi tulizorithishwa unategemea ushiriki wa kila mmoja wetu katika kuzitunza, kuzihifadhi na kuzilinda.

***41. Mheshimiwa Spika*****,** ulinzi, uhifadhi na uendelevu wa maliasili zetu ni matokeo ya ushirikiano wa karibu kati ya Serikali na wananchi. Kwa msingi huo, nitumie fursa hii kuwapongeza wananchi wote hususan wale wanaoishi karibu na maeneo yaliyohifadhiwa ambao wamekuwa wakitoa mchango mkubwa katika kufanikisha uhifadhi, ulinzi na uendelezaji wa maliasili zetu.

***42. Mheshimiwa Spika*****,** sambamba na mafanikio hayo, katika siku za hivi karibuni tumeanza kushuhudia matukio ambayo hatujayazoea kwenye maeneo yetu. Matukio hayo, yanahusisha baadhi ya wananchi wanaoishi karibu na maeneo yaliyohifadhiwa kuwavamia kwa silaha askari wetu wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Jeshi la Uhifadhi wa Misitu wanapokuwa wakitekeleza majukumu yao ya ulinzi. Matukio hayo yamekuwa yakitokea pindi askari hao wanapokuwa wakikamata mifugo iliyoingizwa ndani ya hifadhi kwa ajili ya malisho ama kupambana na majangili wanaokutwa ndani ya maeneo ya hifadhi kinyume cha sheria. Vitendo hivi vya uvunjifu wa sheria haviwezi kuvumilika na Serikali itachukua hatua stahiki za kisheria kwa wale wote watakaokutwa na hatia ya kujihusisha na uvunjifu huo wa sheria. Nitumie fursa hii kuelekeza Mamlaka za Uhifadhi kuendelea kushirikiana na wananchi kwenye maeneo yote kwa kutoa elimu ya ulinzi shirikishi na kulinda maeneo yaliyohifadhiwa.

***43. Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha migogoro hii inakoma na kutojirudiarudia ninaelekeza Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi na kushirikiana nao katika nkuhakikisha operesheni zinazoendeshwa hazileti athari za migongano miongoni mwa makundi mbalimbali kwenye maeneo ya jirani na hifadhi.

***44. Mheshimiwa Spika***, vilevile, niwasihi Waheshimiwa Wabunge wenzangu hususan wale wanaotoka jirani na maeneo ya hifadhi kuendelea kuwaelimisha wananchi katika maeneo yetu kuhusu umuhimu wa kutunza maliasili tulizonazo kwa faida yetu na vizazi vijavyo. Suala la uhifadhi wa maliasili lipeni kipaumbele kwenye mikutano na wananchi wenu sambamba na kusisitiza utii wa sheria bila shuruti.

**HITIMISHO**

***45. Mheshimiwa Spika***, wakati nikielekea kuhitimisha hotuba yangu nikushukuru tena wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kutuongoza vizuri katika kipindi chote cha mkutano huu wa kumi. Kipekee kabisa, ninamshukuru Bi. Nenelwa Mwihambi, Katibu wa Bunge, pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha mkutano huu.

***46. Mheshimiwa Spika***, ninawashukuru pia, wale wote waliokuwa na jukumu la ulinzi na usalama katika kuhakikisha mkutano huu unafanyika na kumalizika salama salimini. Shukrani zangu za dhati ninazielekeza kwa madereva wote mliotekeleza wajibu wenu kwa ufanisi mkubwa bila kuwasahau waandishi wa habari kwa kuendelea kuuhabarisha umma wa Watanzania kile kilichokuwa kikiendelea hapa Bungeni.

***47. Mheshimiwa Spika***, shukrani zangu za mwisho ni kwa wananchi wa Dodoma hususan Jiji la Dodoma ambao wametuonesha ukarimu mkubwa ikiwa ni pamoja na kutupatia huduma zote muhimu na hivyo kutuwezesha kukamilisha mkutano huu kwa mafanikio makubwa. Vilevile, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano mkubwa mnaonipatia katika kipindi chote cha Bunge, na nitumie nafasi hii sasa kuwatakia wote safari njema wakati mnarejea katika maeneo yenu ya uwakilishi.

***48. Mheshimiwa Spika***, sote tunafahamu kwamba mwishoni mwa mwezi huu baadhi ya ndugu zetu Wakristo wataanza kipindi cha Ibada ya Mfungo na Toba yaani **Kwaresma**. Kadhalika, katika wiki ya mwisho wa mwezi ujao ndugu zetu Waislamu wataingia kwenye kipindi cha Ibada ya Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa **Ramadhan**. Hivyo basi, nitumie nafasi hii kuwatakia heri wale wote watakaojaaliwa kutekeleza Ibada hizo. Aidha, niwaombe kutumia vema kipindi hicho cha mfungo kuliombea Taifa letu ili Mwenyezi Mungu atuepushe na majanga na atujalie mafanikio zaidi.

***49. Mheshimiwa Spika***, mwisho, kabla ya kutoa hoja ya kuahirisha Bunge hili, ninawatakia kila la heri wawakilishi wa Tanzania katika hatua za makundi ya Klabu Bingwa Afrika na Shirikisho katika michezo yao ya ugenini. Tunaitakia kila heri

klabu ya Dar Young African inayocheza michezo ya Shirikisho tarehe 12 Februari 2023 huko Tunisia. Ujumbe wetu kwao tetemesha Watunisia. Vilevile, tunaitakia heri nyingi sana Simba Sports Club wekundu wa msimbazi wanaocheza michezo ya klabu bingwa Afrika huko Guinea tarehe 11 Februari, 2023. Ujumbe wetu kwenu nyunyiza hao wa Guinea walale magoli mengi kwao. Hatuna mashaka na viwango vyenu, Simba nyie ni miongoni mwa vilabu 10 bora Afrika.

***50. Mheshimiwa Spika***, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako tukufu sasa liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 04 Aprili, 2023 litakapokutana tena saa 3.00 asubuhi hapa jijini Dodoma.

***51. Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.